**JAMHURI YA MUUNGO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**638** **VIELELEZO NA TEKNOLOJIA**

**Muda: Saa 3 Hours** **Mwaka: 2024**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina Sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na manne (14).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka Sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka Sehemu **B**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na Sehemu **B** ina alama sitini **(60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA



Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Eleza mambo muhimu ya kuzingatia katika kufaragua na kutengeneza zana zinazoendana na malengo mahsusi.
2. Eleza kwa ufupi vigezo vinne vya kutumia katika kuandaa mchoro wa pembe tatu kwa ajili ya kufundishia wanafunzi wa darasa la pili.
3. Eleza kwa nini vielelezo na teknolojia asilia havitumiki katika ufundishaji na ujifunzaji wa sasa.
4. Toa hoja nne kuhusu vigezo vinavyoweza kutumika katika kutathmini chati bora ya kufundishia na kujifunzia.
5. Chambua faida nne za walimu kutumia vielelezo na teknolojia vyenye kukuza uwezo wa udadisi na kufikiri kwa wanafunzi.
6. Thibitisha kauli kwamba "njia ya kununua zana inatakiwa kuwa ya mwisho kati ya njia za upatikanaji wa zana za kufundishia na kujifunzia."
7. Eleza kwa kifupi sababu nne zinazowafanya walimu wasitumie kompyuta kama zana ya kufundishia na kujifunzia.
8. Chambua matumizi ya vielelezo na teknolojia maono katika kusaidia walimu kurahisisha zoezi la ufundishaji.
9. Eleza kwa kifupi tofauti kati ya vielelezo na teknolojia kisasa na vielelezo na teknolojia asili katika ufundishaji na ujifunzaji.
10. Pendekeza njia zitakazowawezesha walimu kutengeneza vielelezo na teknolojia vinavyoweza kuibua vipaji kwa wanafunzi.

## SEHEMU B (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

11. Kwa kutumia hoja tano, eleza hatua sita za kufuatwa na wanafunzi wa darasa la sita kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia.
12. Fafanua njia tano zitakazowawezesha walimu kutunza vielelezo na teknolojia vya kufundishia na kujifunzia.
13. Kubaliana na kauli kwamba "walimu hukumbana na changamoto mbalimbali zinazowafanya washindwe kutengeneza vielelezo na teknolojia vya kufundishia na kujifunzia."
14. Chambua faida tano za kutumia vielelezo na teknolojia masikizi katika ufundishaji na ujifunzaji


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org